

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA WAZIRI MKUU - KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU KWA KUSHIRIKIANA NA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KUPITIA MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA (TEA)

TAARIFA KWA UMMA

TANGAZO LA MAOMBI YA MAFUNZO YA KUENDELEZA UJUZI KWA VIJANA WENYE ULEMAVU KUPITIA UFADHILI WA MFUKO WA KUENDELEZA UJUZI

- 1.0 Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), inapenda kuutangazia umma wa Watanzania kuhusiana na ufadhili kwa ajili ya kuendeleza ujuzi kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Lengo ni kuwezesha Watu wenye Ulemavu kujiajiri au kuajiriwa ili kuchangia katika pato la Taifa. Mafunzo ya kukuza ujuzi yatafanyika katika vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa watu wenye ulemavu vinavyomilikiwa na Serikali ambavyo ni Sabasaba (Singida), Mirongo (Mwanza), Yombo (Dar es salaam), Masiwani (Tanga) na Luanzari (Tabora). Ujuzi utakaotolewa utajikita katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026).
- 2.0 Ufadhili huu wa mafunzo ya kuendeleza ujuzi ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ujuzi na Stadi za Kazi kwa ajili ya ajira zenye Tija (Education and Skills for Productive Jobs-ESPJ) ambao unasimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) na unapata ufadhili wa pamoja kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia. Programu ya ESPJ ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi (National Skills Development Strategy – NSDS: 2016-2021). Mafunzo husika yatafanyika kwa muda wa miezi mitatu na gharama za mafunzo zitaghaharamiwa na Serikali kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (Skills Development Fund-SDF) unaosimamiwa na TEA.
- 3.0 Fani za mafunzo ya kuendeleza ujuzi zitakazotolewa ni Utengenezaji wa Batiki; Kilimo cha Bustani (Horticulture); Mapambo ya Ukumbini; Uchomeleaji na Uungaji Vyuma; Ufundi wa Simu; Umeme wa Majumbani; Uokaji wa Mikate na Keki; Upishi; Urembo; Useremala; Ushonaji wa Nguo; Ushonaji wa Nguo na Mitindo; na Ususi na Urembo.

4.0 Vijana wenye ulemavu wenye sifa zifuatazo wanataarifiwa kuomba kupata mafunzo husika: -

- (i) Awe amesajiliwa katika rejesta ya Watu wenye Ulemavu inayopatikana katika Halmashauri zote nchini.
- (ii) Awe mwenye umri kati ya miaka 15 hadi 40.
- (iii) Awe hajawahi kupata mafunzo ya kukuza ujuzi katika vyuo mbalimbali nchini.
- (iv) Awe Mtanzania, mwenye kitambulisho cha Taifa (NIDA), Kadi ya Mpiga Kura au barua ya utambulisho ya Serikali ya kijiji/mtaa.

5.0 Utaratibu wa kutuma maombi :-

- (i) Fomu za maombi zinapatikana katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri kupitia Afisa wa Ustawi wa Jamii na katika vyuo vya mafunzo vya watu wenye ulemavu vilivyoainishwa katika aya ya 1.
- (ii) Fomu zitakazojazwa ni lazima zisainiwe na kugongwa muhuri na Mtendaji wa Mtaa/Kijiji na Afisa wa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri.
- (iii) Fomu za maombi ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri husika kwa Afisa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu-Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa uchambuzi.
- (iv) Waombaji wanashauriwa kuchagua vyuo vilivyo karibu na maeneo wanayoishi.

6.0 Vijana watakaochaguliwa wataarifiwa kupitia matangazo mbalimbali katika vyombo vya habari na mbao za matangazo za Halmashauri, na Tovuti ya www.kazi.go.tz pamoja na Tovuti ya www.tea.or.tz.

7.0 Muda wa maombi ni kuanzia tarehe **29 Agosti** hadi **07 Septemba 2022**.

8.0 Kwa ufafanuzi na maelezo zaidi wasiliana na: Mratibu wa Vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu kwa namba ya simu: 0755906018 au barua pepe suzana.mayengo@kazi.go.tz

Imetolewa na:

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (OWM-KVAU)

29 AGOSTI 2022